# Biashara Leo

ISSN 000-000 No 1

Yaliyomo

Habari

**Usafiri wa Daladala ni kero, Mwanza**

Watumiaji wa usafiri wa daladala jijini Mwanza wamewalalamikia wasafirishaji wa abiria kwa kukatisha safari zao.

Uk. 2

Habari

**Hofu ya usalama DRC yaathiri biashara ya dagaa**

Imefahamika kuwa hofu ya usalama ndiyo chanzo cha wafanyabiashara wa Kitanzania kutothubutu kufanya biashara katika nchi za kiafriaka.

Uk. 4

Makala

**Mwaloni:Chachu ya ajira jijini Mwanza**

Soko la kimataifa Mwaloni lililoko jiijini Mwanza limekuwa ni chachu ya maendeleo kwa kutoa ajira kwa vijana na makundi mbalimbali ya kijamii jijini.

Uk. 6

# Soko la Mwaloni laajiri vijana 600 Mwanza

Na David Azaria



*Baadhi ya vijana wakiwa katika shughuli za samaki katika soko la Mwaloni (Picha na David Azaria)*

Soko la Kimataifa la Samaki la Mwaloni lililoko Katika Jiji la Mwanza limefanikiwa kutoa ajira kwa zaidi ya Vijana 600, ambao wanajishughulisha na shughuli mbalimbali ikiwemo ubebaji wa mizigo na kujipatia kipato cha kuendesha maisha yao ya kila siku.

Mbali na vijana hao pia limetoa ajira kwa wanawake wajane, pamoja na wale walioachwa ama kutelekezwa na waume zao, ambao wamekuwa wakifika katika soko hilo na kufanya shughuli na kujipatia fedha za kuweza kusaidia familia zao kwa malazi, chakula, mavazi pamoja na kusomesha.

Katika mahojiano maalum na *Biashara Leo*, Mwenyekiti wa wafanyabiashara hao, Christopher Wankyo, alisema soko hilo limesaidia kutengeza ajira kwa vijana na wakina mama ambao kama soko lisingekuwepo wangekuwa na hali ngumu.

Wankyo alisema zaidi ya watu 1000 wanajihusisha na shughuli za kibiashara katika soko hilo kila siku, huku akibainisha kuwa robo tatu ya watu hao ni vijana wenye umri kati ya miaka 18 na 35 ambao wamekuwa wakijihusisha na shughuli za upakuaji na upakiaji pamoja na usombaji wa mizigo mbalimbali.

Inaendelea Uk. 2

## Masharti magumu yakwamisha wajasiriamali Mwanza

Na Julieth Mkireri

Mashariti yanayotolewa na baadhi ya Taasisi za fedha yamedaiwa kuwa moja ya changamoto zinazowakwamisha wakinamama wajasiriamali wanaofanya shughuli za kibiashara katika soko kuu jijini Mwanza kupata mikopo.

Mkazi wa Ilemela Jijini Mwanza Jenifa Adam (36) alisema kuwa ameshindwa kuwa na biashara kubwa kutokana na kukosa mtaji na hivyo kuendelea kubaki kufanya biashara ndogondogo.

"Hizi taasisi zinazotoa mikopo zinaweka masharti magumu kiasi kwamba tunashindwa kupata mikopo ya kuendeleza shughuli zetu za ujasiriamali tunaomba walegeze masharti ili tuweze kukopa na kuendeleza biashara zetu" alisemaJenifa.

Naye mjasiriamali Veronika George alisema kuwa uwepo kwa masharti magumu kwenye baadhi ya taasisi zinazotoa mikopo imemsababishia kutotimiza Malengo ya kukuza biashara yake.

Inaendelea Uk. 2

## Wananchi waiomba serikali kutaifisha viwanda"mfu" Mwanza

Na Paulina David

Baadhi ya wananchi jijini Mwanza wameishauri serikali kuvitaifisha viwanda mbalimbali ilivyoviuzwa kwa wawekezaji na kushindwa kufanya kazi ili kusaidia kutatua tatizo la ajira nchini.

Baadhi ya viwanda vilivyobinafsishwa na havifanyi kazi mkoani Mwanza ni kiwanda cha Ngozi kilichopo wilayani Ilemela ambacho ni moja ya viwanda vilivyoajiri watu wengi mkoani Mwanza.

Mkazi wa eneo la Nyakato, Juma Musa alisema sekta ya viwanda hutoa ajira kwa watu wengi lakini baada ya serikali kuviuza viwanda vyake kwa wawekezaji ambavyo kwa sasa vimefungwa badala ya kufanya kazi.

"Tunaiomba serikali ichukue hatua kwenye hili, ivitaifishe viwanda vyote ilivyoviuza na kufungwa ili vianze kufanya kazi ya uzalishaji kama ilivyokuwa zamani,"alisema Juma

Alisema kuwa Viwanda hivyo vitasaidia kutoa ajira kwa watanzania na serikali kupata mapato hali ambayo itasaidia kuboresha maisha ya watanzania na hali ya uchumi wa taifa.

Inaendelea Uk. 3

Gazeti hili Limetolewa na Wanamafunzo wa Habari za Uchunguzi za Biashara SAUT

# ... soko la Mwaloni

Inatoka uk. 1

"Kazi nyingi katika soko hili ni za kutumia nguvu na ndiyo maana unaona vijana ndio wengi ndani ya soko hili kwa sababu inaaminika kwamba wana nguvu, kwa hiyo kila siku soko linatengeneza ajira kwa zaidi ya vijana 600 ambao hawa wanapata fedha zao taslimu kila siku baada ya kazi……" alisema Mwenyekiti huyo.

Wankyo aliongeza kuwa kuna akina mama hapa ambao wengi wao ni wajane, wapo pia walioachwa na kukimbiwa na waume zao, nao wanafanya biashara za aina mbalimbali ndani ya soko ikiwa ni pamoja na kuuza mbogamboga, dagaa, na samaki na kujipatia fedha za kujikimu kimaisha…..".

Baadhi ya vijana wanaojishughulisha na biashara pamoja na shughuli mbalimbali ndani ya soko hilo ikiwemo upakuaji na upakiaji wa mizigo bandarini,walisema uwepo wa soko hilo umewafanya kujipatia ajira za kudumu ambazo zinawafanya kumudu gharama za maisha ya kila siku.

"Kwa mfano mimi hapa kazi yangu kila siku ni kukatakata vichwa vya samaki vinavyotoka kiwandani kwa ajili ya kuandaliwa kabla ya kukaushwa na kupelekwa kwa walaji, naingia asubuhi saa 12 natoka saa 12 jioni au saa moja usiku wakati mwingine hadi saa mbili,lakini ninapotoka hapa nakuwa na fedha yangu taslimu ambayo ni mali yangu kwa kazi nilizofanya siku nzima…." Alisema Mmoja wa vijana hao Enos Lucas.

Aliongeza"hapa kama mzigo unakuwa mkubwa sana kwa siku naondoka na shilingi 40,000/=,au 50,000/=,pamoja na kwamba kazi ni ngumu lakini fedha inayopatikana ni nzuri na inasaidia kuendesha maisha ya kila siku kwa sababu tuna familia ambazo zinatutegemea……'' anasema..

Kwa upande wao John Elias, Zakayo Kingi, na Mabula George wanasema uwepo wa soko hilo umewafanya kupata ajira kwani fedha wanazozipata zimekuwa zikiwasaidia kuendesha maisha yao ikiwa ni pamoja na kusomesha watoto wao pamoja na wadogo zao.

"Kama hili soko lisingekuwepo sijui sasa hivi ingekuwaje, vijana tuko wengi sana humu ndani na tunapata fedha za kutosha kabisa, kama mtu unajituma huwezi kukosa shilingi 20,000/= kwa siku au 40,000/=, na kwa sababu ukitoka hapa unakuwa umechoka unakwenda nyumbani kupumzika hakuna starehe, na kama hili soko lisingekuwepo basi hali ingekuwa ni tete huko mitaani, ingekuwa ni wizi mtindo mmoja….." alisema Mabula.

Baadhi ya wakina mama wanaojishughulisha na shughuli mbalimbali ikiwemo ubebaji wa mizigo katika soko hilo, walisema uwepo wa soko hilo umewasaidia kujipatia fedha za kuendesha maisha ya familia zao bila kutegemea wanaume.

"Kila siku kazi yangu kubwa ni kusomba vichwa vya samaki na kuleta kwa hawa wakataji, ninapotoka jioni natoka na shilingi zangu 30,000/=,wakati mwingine 40,000/= ambazo zinatosha kabisa kuwalisha watoto wangu watatu ambao ninaoishi nao nyumbani kwangu Igogo nilipopanga,ndivyo maisha yanavyokwenda…'' alisema Getruda Joram ambaye ni Mama Mjane.

Soko la Mwaloni lilijengwa na Halmashauri ya jiji la Mwanza na kuanza kufanya kazi mwaka 2005, ambapo soko hilo limekuwa kituo kikuu cha uzalishaji wa samaki aina ya Sangara wakavu na wale wa Kubanikwa pamoja na dagaa ambao soko lao kubwa liko nje ya Nchi ikiwa ni pamoja na Jamhuri ya Kidemokrasia ya watu wa Kongo,Msumbiji, Burundi na Rwanda.

# Usafiri wa Daladala ni kero, Mwanza

**Na Mustapha Kapalata na Lucas Edward**

Watumiaji wa usafiri wa daladala jijini Mwanza wamewalalamikia wasafirishaji wa abiria kwa kukatisha safari zao.

Akizungumza kwa nyakati tofauti na gazeti hili mmoja wa watumiaji wa usafiri huo, Mwinyi Abdallah, alisema kuwa baadhi ya madereva hao wamekuwa na mazoea ya kukatisha safari na kusababisha kulipa nauli mara mbili.

"Mfano daladala inayotoka Malimbe inatakiwa ifike mjini badala yake inaishia kona ya Nyegezi na hivyo kutulazimu abiria kutafuta usafiri mwingine jambo ambalo linatupotezea muda na kutuongezea gharama ya usafiri mara mbili," alisema Mwinyi.

> **"Mfano daladala inayotoka Malimbe inatakiwa ifike mjini badala yake inaishia kona ya Nyegezi na hivyo kutulazimu abiria kutafuta usafiri mwingine"**

Naye, Fatuma Athumani mkazi wa Igoma alisema kuwa , baadhi ya magari yanayotoa huduma ya usafiri wa kutoka Igoma kwenda Ilemela mara nyingi hukatisha safari zake kwa kuangalia eneo lenye abiria wengi.

"Hebu angalia kwa mfano wakati wa asubuhi abiria wengi wanaotoka maeneo ya Igoma hivyo magari yanayotoka huko kwenda Ilemela huishia njiani ili kuwawahi abiria tena wa Igoma;"alisema na kuongeza.

"Abiria aliyekuwa anaenda Ilemela hulazimika kupanda gari nyingine na kulipa nauli nyingine jambo ambalo husababisha kuingia gharama mara mbili na kupoteza muda wa kutafuta gari lingine,' .

Mmoja wa madereva wa daladala inayofanya safari zake kutoka Igoma kuelekea Buhongwa jijini Mwanza Abibu Juma alikiri kuwepo kwa tatizo hilo kwa baadhi ya daladala hali ambayo inapunguza kipato kwa daladala husika kutokana na wimbi kubwa la daladala zinazokatisha safari zao.

"Kila siku tunatakiwa kuwasilisha shilingi elfu arobaini lakini kutokana na vitendo vya kukatisha safari tunajikuta hatufikishi malengo hayo kitu ambacho hutuletea migogoro na wamiliki wa daladala zetu" alisema Habibu

Akizungumzia swala hilo Kaimu Meneja wa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi kavu na Majini (SUMATRA) Michael Polycarp alikiri kuwepo kwa tatizo hilo na kusema kuwa jitihada mbalimbali zinafanywa ili kuhakikisha vyombo hivyo vya usafiri vinafanya safari zake kama zilivyopangiwa.

Aidha alisema kuwa mamlaka hiyo inashirikiana na jeshi la polisi katika kukabiliana na tatizo na kusisitiza kuwa dereva atakayebainika kukatisha njia atachukuliwa hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kufikishwa mahakamani kama sheria zinavyoeleza.

# Mashariri magumu, wajasiriamali Mwanza

Inatoka uk. 1

Walitaja baadhi ya changamoto hizo kuwa ni pamoja na kutakiwa dhamana kubwa kabla ya kupatiwa mikopo kutoka katika taasisi hizo na hasa mabenki.

Wajasiriamali hao wametoa wito kwa taasisi za fedha kulegeza Masharti ya mikopo ili waweze kupata fursa za kukopa na kuboresha biashara zao hali ambayo itawawezesha kuwa na mitaji ya kuendeleza biashara zao kwa ngazi ya kitaifa na kimataifa.

Hata hivyo akifafanua juu ya changamoto hiyo mmoja wa wajumbe wa bodi ya SACCOS ya wafanyabiashara ndogondogo wa Kirumba (WADOKI) ambaye hakupenda kutajwa jina lake Gazetini alisema kuwa wajasiriamali wengi hawana utaratibu wa kujiwekea fedha kwenye vyama vya kuweka na kukopa (SACCOS).

Alisema masharti yanayotolewa kwenye SACCOS ni rahisi kwa mwananchama kwa sababu riba yake ni ndogo jambo ambalo lingewasaidia wajasiriamali hao kupata mikopo na kupata mitaji ya kuendeleza biashara zao.

"Changamoto kubwa kwa hawa wajasiriamali wetu ni kutojiwekea mitaji kwenye SACCOS zinazotoa mikopo na wengi wao hawapendi kununua hisa kujiwekea mtaji na hivyo kuendelea kulalamikia masharti wanayopewa pindi wanapoomba mkopo" alisema mjumbe huyo wa Bodi.

Alifafanua kuwa SACCOS hizo huweka Masharti ya kutoa mikopo ili kujiwekea ulinzi wa fedha wanazokopesha kwa waombaji na kutoa mfano kuwa zipo baadhi ya SACCOS ambazo zilikuwa zimelegeza masharti ya kutoa mikopo na fedha zao zilipotea kwa kutokuwa na utaratibu wa kuwabana wakopaji.

Kwa mujibu wa Mjumbe huyo wa Bodi ya WADOKI ambaye pia ni mfanyabiashara katika jiji la Mwanza, changamoto nyingine inayodaiwa kuwakabili wajasiriamali hao ni kutokuwa na nyumba wanazomiliki wenyewe na hivyo kukosa fursa ya kutimiza masharti ya mkopaji anayetakiwa kuweka nyumba kama dhamana.

## Viwanda "mfu" Mwanza

Inatoka uk. 1

Naye mkazi wa Kilimahewa, Halima Hamisi alisema baadhi ya wananchi walikuwa wakiendesha biashara zao kwa kuuza chakula kwa wafanyakazi wa viwandani huku wengine wakitegemea ajira kutokana na kuuza bidhaa zinazozalishwa viwandani lakini baada ya viwanda hivyo kufungwa wamepoteza kazi.

Akizungumzia madai hayo Ofisa biashara wa jiji la Mwanza, John Peter alisema ni kweli kufungwa kwa viwanda vilivyouzwa na serikali kwa wawekezaji kumesababisha hasara kwa taifa na kuongeza tatizo la ukosefu wa ajira kwa watanzania.

Alisema kufungwa kwa viwanda hivyo kumeisababishia serikali kukosa mapato kutoka kwenye mishahara ya wafanyakazi , kodi za uzalishaji wa bidhaa pamoja na kodi za viwanda .

Aliongeza kuwa ili kutatua hali hiyo ni lazima serikali itazame upya juu ya sera zake na kuchukua hatua ambazo zitasaidia kuweka msukumo kwa wawekezaji walionunua viwanda ili viweze kuanza kazi.

Akifafanua Ofisa biashara alisema hatua hiyo itawasaidia wakulima wa pamba kuuza pamba yao ndani ya nchi na kuuza nguo nje ya nchi huku wauzaji wa ngozi kuuza ngozi zao viwandani badala ya kuzisafirisha nje ya nchi kabla hazijaongezwa thamani.

Kwa mujibu wa ofisi ya takwimu ya Taifa hadi kufikia Desemba mwaka 2011 zaidi ya watu milioni 2 wenye uwezo wa kufanya kazi nchini hawana ajira.

# SAUT yaleta neema kwa majirani

*"Hebu fikiria kwa mtu ambaye alikuwa akitegemea auze mahindi ya kuchoma ili apate pesa kidogo akanunue unga au mchele ili familia ipate chakula leo wanunuzi hawapo huko nyumbani hali itakuwa je,?"*

Wananchi wanaokizunguka chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino (SAUT) kilichopo Nyegezi jijini Mwanza wamenufaika na ajira mbalimbali zinazopatikana na uwepo wa chuo.

Mfanyakazi katika chuo hicho, Asteria Alcardo alisema asilimia kubwa ya wananchi anaoishi karibu na chuo hicho,wanafanya kazi mbalimbali zikiwamo za usafi katika chuo hicho, kufua nguo za wanachuo na kufanya biashara ndogo ndogo.

Alisema kuwa hatua hiyo imewawezesha kupata kipato ambacho kinawasaidia kuendesha maisha yao na familia zao.

Aliongeza kuwa uwepo wa chuo hicho, kumesababisha baadhi yao kupunguza safari za kwenda kutafuta vibarua na biashara ndogo ndogo katika maeneo ya mjini.

Aidha alidai baadhi ya watu wanaofanya bishara ndogondogo katika chuo hichi huyumba kiuchumi wakati chuo hicho kufungwa.

Naye, Heleni Kalambo ambaye ni mfanyakazi katika duka la vifaa la mashuleni na maofisini eneo la Nyamalango iliyopo jirani na chuo, alitoa wito kwa wakazi wa maeneo yanayozunguka eneo hilo kubuni namna nyingine ya kujiingizia kipato ili waweze kuendesha maisha yao pindi chuo kinapofungwa.

"Ndugu mwandishi usione hivi, sasa baadhi ya wakazi wa mtaa huu wanaishi kwa shida kwa hizi wiki mbili tatu tu ambazo chuo kimefungwa," alisema.

"Hebu fikiria kwa mtu ambaye alikuwa akitegemea auze mahindi ya kuchoma ili apate pesa kidogo akanunue unga au mchele ili familia ipate chakula leo wanunuzi hawapo huko nyumbani hali itakuwa je,?" alisema na kuhoji Bi Kalambo

Wanafunzi wa Chuo kikuu cha Mt Agostino SAUT walianza kuondoka maeneo ya chuo kuanzia tarehe 3 mwezi mara baada ya kumaliza mitahani yao ya muhula wa pili.

# Hosteli kulipia kodi jiji

**Na Mustapha Kapalata na Lucas Edward**

Halmashauri ya Jiji la Mwanza limeazimia kukusanya kodi kutoka kwenye hosteli zinazotumiwa na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino (SAUT).

Afisa Biashara wa jiji Sizya R Sizya amesema kuwa kodi hiyo itakuwa mojawapo ya vyanzo vya mapato ya jiji la Mwanza kwa mwaka huu wa fedha 2012/2013.

Alisema kuwa muda mrefu Halmashauri imekuwa ikipoteza fedha nyingi kwa kutokukusanya mapato katika hosteli mbalimbali wanazoishi wanafunzi wa chuo hicho.

Sizya alisema halmashuri kushirikiana na uongozi wa chuo imeazimia kukusanya kodi kwa wamiliki wa hosteli hizo ambapo kiasi cha asilimia ishirini (20%) kitatozwa kwa kila mwanafunzi atakayeishi hosteli husika.

"Tutahakikisha tunashirikiana na uongozi wa chuo kuwa kila anayemiliki hosteli analipia ili kuongeza pato la jiji ambapo kwa muda mrefu wamekuwa wakiendesha biashara hizo bila kulipia na kuikosesha halmashauri ya jiji fedha nyingi ambapo zingeweza kusaidia katika shughuli za maendeleo" alisema.

Aidha kwa upande wa kiwango cha kodi za nyumba wanazolipa wanafunzi , Sizya, alisema halmashauri haina uamuzi zaidi katika swala hilo kutokana na soko huria ila halmashauri inajaribu kutafuta njia ya kuweza kuweka viwango stahiki kulingana na ubora wa hosteli husika.

Mshauri Msaidizi wa wanafunzi katika chuo hicho, Leonard Nyanzira, alisema kuwa zaidi ya wanafunzi 13000 ambao ni sawa na robo tatu ya wanafunzi wote wanaishi nje ya chuo. "Hosteli za chuo zinachukua wanafunzi waziozidi 1500 na hivyo idadi kubwa ya wanafunzi wapatao zaidi ya 13000 wanaoishi nje ya chuo" alisema

Akiongelea suala la ulipaji wa kodi kwa wamiliki wa hosteli hizo alisema haoni sababu ya serikali kutokukusanya kodi wakati wanaingiza pato kubwa kutokana na hosteli hizo ambapo hosteli nyingi hutoza kuanzia milioni 1 kwa kila mwanafunzi na kubainisha kuwa kuna hosteli zinawanafunzi zaidi ya 100.

Kwa upande mwingine Nyanzira alisema chuo kimeanza zoezi la kuchukua taarifa ya hosteli zinazohudumia wanafunzi kwa mwaka huu wa fedha ili waweze wanafunzi kupata huduma hizo kiurahisi pamoja na taratibu za ulipaji wa kodi uwe mzuri.

Aidha mmoja wa wamiliki wa hosteli katika eneo hilo Hussein Siagi alisema hana taarifa yoyote katika zoezi hilo la ulipaji wa kodi na kukiri kuwa hajawahi kulipa kodi katika hosteli hizo zilioanza kazi zaidi ya miaka 5 iliopita.

Hata hivyo alibainisha kuwa hana tatizo katika ulipaji wa kodi hiyo na kuiomba halmashauri ya jiji izingatie kipato cha hosteli na hali ya ujenzi wa hosteli wakati zoezi litakapoanza.

Hosteli nyingi ambazo wanafunzi wa SAUT wanaishi ziko maeneo ya Malimbe, Sweya, Kuzenza, Bondeni, Nyamalango, Kijiweni, Nyegezi Kona na Nganza.

## Wakulima wa pamba watakiwa kuzingatia ubora

**Na Winfrida Celestine**

Bodi ya pamba nchini imewataka wakulima kuzingatia ubora wa uzalishaji wa zao hilo ili kupata bei itakayowanufaisha na kurejesha gharama za uzalishaji.

Rai hiyo ilitolewa na mkaguzi toka bodi ya pamba nchini (TCB) Bw Buluma Kalidushi wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini Mwanza kuhusiana na uzalishaji wa zao hilo .

Alisema kuwa pamoja na bei ya pamba kushuka kwa bei toka tsh 1000 kwa kilo iliyopangwa awali na kuwa tsh 660 ,na hivyo kusababisha ushukaji wa bei kidunia bado suala la uduni wa zao hilo unachangia hali hiyo.

Aliongeza kuwa baadhi ya wakulima wamekuwa wakishindwa kuhifadhi zao hilo hivyo pamba yao kuwa chafu na isiyo sitahili kuuzwa kwa bei ya juu

"Unajua nawashangaa sana wakulima kwani mtu anachanganya pamba na mawe ili kuongeze uzito .Hakika wanajidanganya kwani teknolojia imekua sana na hakuna anayeweza kununua mawe badala ya pamba." Alisema Kalidushi.

Hata hivyo alisema kwamba kila mwaka Bodi imekuwa ikifanya uzinduzi wa zao hilo ambapo changamoto zinazochangia kushuka kwake hubainishwa.

Baadhi ya wakulima wa zao hilo waliozungumza na waandishi kwa nyakati tofauti walisema serikali inapaswa kusaidia wakulima katika uzalishaji bora wa zao hilo."Tangia viwanda vya nguo vifungwe hapa nchini zao la pamba linaonekana kutothaminiwa huku serikali ikiipa kisongo na ndiyo sababu ya kuanguka kwake." Alisema Kija Shija.

Bei ya zao la pamba imekuwa ikishuka mwaka hadi mwaka kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuporomoka kwa thamani ya zao hilo kwenye soko la dunia.

Hadi sasa mikoa inayoongoza kwa uzalishaji wa zao hilo ni ya kanda ya ziwa ikiwemo Mwanza na Shinyanga inayouza katika viwanda vya ndani na nje ya nchi.

# Hofu ya usalama DRC yaathiri biashara ya dagaa

Na Godwin Msalichuma

Imefahamika kuwa hofu ya usalama ndiyo chanzo cha wafanyabiashara wa Kitanzania kutothubutu kufanya biashara katika nchi za kiafriaka.

Mfanyabishara wa dagaa kutoka DRC Bw. John Ngala alisema kuwa wafanyabiashara wa Kitanzania wameshindwa kupata fursa ya kupeleka dagaa DRC na nchi nyingine za Kiafrika kutokana na mapigano katiaka maeneo hayo.

Ngala alisema kuwa amani, upendo na utulivu na mazingira ya kuridhisha ya ufanyaji biashara mbali na matatizo mengine yaliyoko Tanzania, kwa upande wa kwao hakuna.

"Najua Watanzania wengi wanaogopa mapigano kwa kuwa wao hawakuzoea na ndicho kinachowafanya washindwe kuleta dagaa katika nchi yetu…ni ukweli usiofichika hali iliyoko huku kwenu siyo ile ya kwetu hatuna ushirikiano mzuri na watu wa kutoka nje ya DRC" alisema mfanyabiashara huyo wa dagaa.

Naye mfanyabiashara wa dagaa wa Kitanzania sokoni Bw. Issa Silvery alisema kutokana na amani kuwa ndogo DRC na ushirikiano mdogo wakiwa huko imewalazimu kuwaachia waendelee kunufaika na uwepo wa soko hilo la dagaa na wao kuambulia kazi za upakiaji katika malori.

"Hatujazoea mitutu bwana acha tuendelee na kazi hizi tunazozipata hapa za ushindiliaji na upakiaji katika malori maana zaidi ya watu 3,000 kwa siku tunapata vibarua sokoni hapa…..kwani tunaogopa kuthubutu kwenda huko kwao isitoshe waliobahatika kufika walikiona cha mtemakuni" alisema Bw. Silvery bila kufafanua.

Aidha mwenyekiti wa soko hilo, Christopher Wankyo alithibitisha kuwepo kwa wafanyabiashara kutoka DRC na jinsi wanavyochangamkia uwepo wa soko hilo la dagaa kinyume na wenzao wa Kitanzania.

"Tunapokea wafanyabiashara wengi kutoka DRC kutokana na hali ya utulivu na amani na pia upendo na ushirikiano wetu tunaounyesha kwao hili ni kinyume ukienda kwao na wao wanasema dhahiri ya kwamba kwao amani ni tete" alisema mwenyekiti huyo.

Akieleza faida, Mfanyabishara kutoka DRC Bw. John Ngala alisema kuwa biashara ya dagaa inaendelea kuwapa faida kubwa kwani wao wanawapata kwa bei ya dola 160 za kimarekani kwa gunia ambazo ni sawa na sh.256,000 ukilinganisha na bei wanayouzia kwao ambayo ni dola 300 ambazo sawa na sh. 480,000 kwa gunia moja.

"Biashara hii imekuwa na mafanikio kwetu ndiyo maana unaona tunaendelea nayo mpaka leo hii….tunapata mzigo kwa bei nzuri ya dola za kimarekani 160 na kule tunaenda kuuza kwa wateja wetu kwa dola 300 kwa gunia moja la dagaa " alisema kwa kujigamba Bw. Ngala.

Alisema kuwa hawaishii kuuza ndani ya DRC tu bali wamekuwa wakipata wateja kutoka upande wa Congo Brazavile na Angola na imekuwa ikiwachukua muda mfupi wa kurudi tena Mwanza kuchukua mzigo mwingine kwa ajili ya wateja wao.

# Ukarabati wa barabara waleta msongamano Mwanza

Na Rodrick Mushi

Ubovu wa barabara katika eneo la VOIL, Igogo kwenye barabara kuu inayotoka Mwanza kuelekea Shinyanga imesababisha kero kwa abiria wanaotumia barabara hiyo.

Wakizungumza na gazeti hili, wafanyabiashara wa matunda walisema kuwa ubovu huo wa barabara umekuwa ukisababisha msongamano mkubwa wa magari,jambo ambalo limekuwa likiwasababisha kushidnwa kuwahisha bidhaa hizo masokoni.

Mmoja wa mwananchi, Alex John alisema kuwa eneo hilo la barabara ambalo kwa sasa linafayiwa ukarabati limekuwa likiharibika mara kwa mara na kurudia katika hali yake, kutokana na kutengenezwa chini ya kiwango.

"Eneo la Igogo ambalo linasababisha foleni ya magari limekuwa likiharibika mara kwa mara tangu kutengenezwa kwa hiyo barabara,lakini cha kushangaza ni kwamba mamlaka ya barabara inashindwa kupaboresha ili tatizo hilo lisitokee tena"Alisema Alex.

Mbali na wafanyabishara hao wananchi wa kawaida ambao wanategemea barabara hiyo kusafiri maeneo mbalimbali, walisema kuwa foleni katika barabara hiyo kuu imekuwa kubwa na wakati mwingine wanalazimika kushindwa kusafiri unapofika wakati wa jioni na mwisho wa wiki.

Mmoja wananchi ambaye hakutaka jina lake liandikwe gazetini alisema kuwa adha inayosabishwa na eneo hilo dogo la barabara ambalo ni bovu ni kubwa, kwa wasafiri wanaosafiri maeneo ya airport kuelekea Buhongwa,na Igoma kuelekea Buhongwa.

Wananchi wengine ambao wanasafiri katika ya mji ambao wanakumbana na adha hiyo ni wale wanaosafi kutoka maeneo ya Mjini kuelekea Nyegezi, Mjini kuelekea Mkolani, Buhongwa pamoja na misungwi.

"Msongamano wa magari, tena ambao siyo walazima unasababisha na eneo dogo tu la barabara ambalo limekuwa likiharibika mara kwa mara na sababu ya maji yanayoambatana na mchana yakitokea milima ya Igogo kukatiza," alisema mwananchi huyo.

Inaendelea uk. 5

## Kilimo cha mkataba chanufaisha wakulima wa pamba Mwanza

Na Nashon Kennedy

Zaidi ya vikundi vya wakulima wa pamba 800 katika wilaya za Misungwi na Kwimba mkoani hapa vimenufaika na kilimo cha mkataba katika zao la pamba .

Hayo yameelezwa jana na wakaguzi wa pamba katika wilaya ya Kwimba, Elisha Kitenge na Misungwi Sillani Kamuti wakati wakielezea mafanikio ya kilimo cha mkataba kwa wakulima wa wilaya hizo kwenye mkutano wa wadau, wakulima na watalaam uliofanyika katika Chuo cha Utafiti wa Kilimo Ukiruguru.

Wamesema kuwa wakulima hao wamenufaika na kilimo hicho kwa msimu mwa mwaka huu. Mkulima wilayani Misungwi Peter Busumbo alisema kuwa kilimo cha mkataba kimekuwa ni mkombozi mkubwa wa uchumi katika kaya zao.

Amesema kuwa wananchi hunufaika na kilimo hicho kwa kupata ruzuku ya dawa kwa mkulima.

"Zamani ilikuwa mkulima anapata shida, analima pamba yake akiwa na wasiwasi ya madawa, lakini kwa mpango huu wa kilimo cha mkataba, wakulima wananufaika sana, ingawa kwa sasa tatizo tunalokabiliana nalo ni kushuka kwa bei ya pamba katika soko", alisema.

Naye, Robert Michael alisema kilimo cha kimemuwezesha kusomesha watoto wake wanne kwa kuwalipia ada.

"Kabla sijajiunga na kilimo hiki cha mkataba hali ya uzalishaji wangu kwa siku za nyuma ilikuwa sio nzuri, lakini kupitia kilimo cha mkataba nimeweza kuwasomesha watoto wangu na kwa msimu huu nimepata jumla ya kilo 350 za pamba kwa ekari moja", alisema Michael na kuiomba serikali ikiendeleze kilimo hicho kwani kimekuwa ni cha manufaa kwa wakulima wa vijijini.

Kwa upande mwingine Mkaguzi wa Pamba wilayani Msungwi, Sillan Kamuti alisema kuwa wilaya yake ina jumla ya vikundi 334 vya wakulima na makampuni saba yanayonunua pamba kwa vikundi hivyo vya wakulima vilivyojiunga kwenye kilimo cha mkataba, na alisema kuwa kimewainua wakulima kiuchumi.

"Makampuni yanayonunua pamba ndiyo yaliyoingia mkataba na vikundi hivyo vya wakulima ambapo hutoa mkopo wa dawa , na katika mkopo huo serikali hulipia kiasi cha sh. 1500 kama ruzuku kwa mkulima, na kumuwezesha mkulima kununua dawa kwa Sh. 3,000 tu", alisema Kamuti.

Aliongeza kuwa katika msimu ujao wa kilimo lengo la wilaya ni kuhakikisha kuwa vikundi ambavyo havijajiunga na mpango wa kilimo cha mkataba vitahamsishwa ili viweze kujiunga na katika msimu wa soko wa mwaka 2012/13 wilaya yake inatarajia kuuza jumla ya tani 2900 ambazo ni sawa 2,900,000 zilizotokana na kilimo cha mkataba.

Aliyataja makampuni yaliyoingia mkataba na vikundi hivyo vya wakulima kuwa ni ICK Cotton Ltd, SM Holding, Mwatex, Birchand, Manawa Ginneries, Afrishian na Nyanza Cooperative Union (NCU).

"Makampuni hayo yanayonunua pamba ndiyo yanayonunua pamba wilayani Kwimba, kwa upande wa NCU kinanunua pamba kwa wanachama walio chini ya vyama vya ushirika", aliongeza Kamuti.

Kwa upande wake, Mkaguzi wa pamba wilayani Kwimba, Ally Kitenge alisema kuwa wilaya yake ina jumla ya vikundi 626, lakini vilivyojiunga na kilimo cha mkataba ni vikundi 113 kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo sababu ya hofu ya kunyang'anywa mazao yao.

"Vikundi hivyo ambavyo havijajiunga vina hofu kuwa baada ya kukomaa kwa pamba watanyang'anywa pamba yao, lakini hata hivyo tumefanya juhudi kubwa ya kuvielimisha vikundi hivyo vya wakulima na matarajio yetu ni kuwa mwakani vikundi vingi vitaweza kujiunga na kilimo hicho cha mkataba", alisema Kitenge na kuongeza kuwa katika msimu huu wa kilimo wilaya ya Kwimba inatarajia kuuza jumla ya tani 18,000 za pamba ambazo ni sawa na kilo milioni 18 za pamba kwa msimu huu wa soko wa 2012/13 kutokana na kilimo cha mkataba.

# ..Msongamano, magari Mwanza

Inatoka uk. 4

Akizungumzia tatizo hilo Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Evarsti Ndikilo alikiri kuwepo kwa tatizo hilo na kusema kuwa jitihada mbalimbali zinafanywa kuhakikisha kuwa tatizo hilo linapatiwa ufumbuzi.

Miongoni mwa mikakati ambayo alisema Serikali imejiwekea kuondoa tatizo la msongamano ni pamoja na kujenga barabara za juu kwenye baadhi ya maeneo, pamoja na kufanya upanuzi wa barabara.

Pia Mkuu huyo alisema kuwa mbali na miradi mbalimbali ya barabara ambayo itajengwa, lakini pia uongozi wa Mkoa upo kwenye mkakati wa kurefusha ruti za mabasi ya abiria ambayo yanafanya ruti fupi,na kufuta baadhi ya vitua vingine ambavyo vimekuwa vikisababisha foleni katikati ya jiji.

# Wanafunzi SAUT waenda likizo, biashara zadorora

**Na Happy Severine**

Kufungwa muhula wa pili wa masomo katika chuo kikuu cha Mtakatifu Augustino (SAUT) kilichopo Jijini Mwanza kumepelekea wafanyabiashara wengi wa Mtaa wa Nyamarango kuyakimbia kwa muda maeneo yao ya biashara na kuhamia maeneo mengine ya biashara.

Hali hiyo imejitokeza mara baada ya kufungwa kwa muhula wa pili wa masomo chuoni hapo, mapunziko hayo yatachukua miezi mitatu kuanzia Julai hadi Oktoba mwaka huu.

Daniel Sambo(30) ambae anajihusisha na biashara ya uuzaji wa vifaa vya ofisi na vitabu vya wanachuo, alisema katika mahojiano na mwandishi wa Biashara Leo kwa wiki mbili sasa toka kufungwa kwa muhula wa masomo, zaidi ya wafanyabiasha 10 wameyahama maeneo yao na kukimbilia maeneo mengine ya Nyakato na Igoma kutokana na kukosa wateja wa biashara zao.

Aidha Sambo alieleza, asilimia kubwa ya wafanyabiashara wa eneo la Nyamarango wanawategemea wanachuo hao kwa kuwa ndio wateja wakuu wa biashara zao, kwa sasa biashara zao zimeanza kudolola na zingine zimesimama kabisa.

“Sisi wafanyabiashara wa eneo hili wateja wetu wakuu ni wanachuo…ila kwa sasa hali tunaiona inazidi kuwa mbaya kwani wateja wetu wameenda likizo ndefu ya miezi mitatu… na ndio maana wengi wetu wameamua kuhama maeneo kwenda sehemu nyingine ili kujitafutia ridhiki”…Alisema.

Hata hivyo Sambo alibaini kuwa kuwepo kwa chuo hicho karibu na maeneo yao kumeweza kuwainua wananchi wengi wa eneo hilo kwa kuwapatia ajira na kuwaongezea kipato ambacho kimeweza kuendesha maisha yao ya kila siku.

Mbali na hilo Sambo alifafanua kuwa biashara zao zimekua zikichanganya kuanzia mwezi January hadi Julai mwishoni lakini kwa miezi ya August, September na Oktoba hali inakuwa ni mbaya kibiashara na kufanya hata mapato yetu kushuka.

Alibainisha kuwa suala zima la kushuka kwa mapato ya wafanyabiashara katika miezi hiyo ya likizo, ni kuwategemea wateja wa aina moja tu.

“Mimi Sambo kipindi cha masomo huwa napata faida ya Tsh mil1.2 kwa mwezi katika biashara ya utoaji huduma ya kifedha na Tsh laki 6 kwa uuzaji wa vifaa vya ofisi…ila mwanzoni wakati naanza biashara sikujua kama nitaweza kukutana na wakati mgumu kibiashara pale vyuo vinapofungwa.

Hata hivyo, Mhadhili wa katika titivo cha uchumi kutoka chuo kikuu cha Mtakatifu Augustino (SAUT) Mwanza Castus Zilala alisema endapo kutakuwepo uwekezaji wa ndani, wananchi wengi wataweza kuwekeza na kuinua mapato yao kuliko kutegemea wageni waje kuwekeza.

# Sanamu ya Samaki yatoa ajira kwa vijana

**Na Innocent Ng’oko**

Sanamu ya Samaki iliyopo katika barabara ya Kenyatta jijini Mwanza imewawezesha wapiga picha zaidi ya 40 kujiajiri kwa kuwapiga picha wageni mbalimbali wanaofika eneo hilo na kujipatia fedha za kuweza kujikimu katika maisha yao ya kila siku.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti baadhi ya wapiga picha hao walisema, kuwa hatua ya Kampuni ya Vic Fish kujitolea kujenga sanamu ya samaki katika barabara ya Kenyatta imewawezesha vijana wengi wanaojishughulisha na kazi ya kupiga picha kujipatia kipato.

Walisema kuwa tangu kuzinduliwa kwa sanamu hiyo mwaka 2009, eneo hilo imegeuka kuwa lenye manufaa kwa wapiga picha wengi wa mitaani kujipatia fedha za kutosha kujikimu katika maisha yao ya kila siku.

Mmoja wa wapiga picha hao David Ernest alisema kazi ya kupiga picha katika eneo la sanamu ya samaki imekuwa ikiwawezesha kujipatia fedha kati ya sh. 15,000-30,000 kwa siku kutokana na idadi kubwa ya watu wanaofika katika eneo hilo kwa lengo la kutalii.

Alibainisha kuwa wastani wa watu 100-200 kutoka ndani ya jiji la Mwanza na wageni amabao wanatembelea Mwanza kutoka nje ya nchi zikiwemo nchi za Kenya, Uganda, Burundi na Rwanda mara kwa mara katika eneo hilo kwa ajili ya kujionea sanamu na kupiga picha za kumbukumbu.

Aidha wapiga picha hao walisema kwa sasa wameanzisha umoja wao unaofahamika kwa jina la Nuru Njema ambao unajuisha wanachama 44 kutoka maeneo mbalimbali ya jiji la Mwanza ambao hufika kila siku katika eneo hilo kwa lengo la kupiga picha za wageni na wenyeji wanaofika katika eneo hilo kwa lengo la kujipatia fedha.

Walisema uamuzi wa kuanzisha kikundi hicho cha wapiga picha katika eneo la sanamu ya samaki ni kwa ajili ya kusaidiana katika matatizo mbalimbali na kuongeza kuwa kila mwanachama analazimika kulipa kiasi cha Tsh.5000 wanapojiunga na chama, ambapo kwa sasa wapo mbioni kukisajili kikundi hicho kwa lengo la kujipatia mikopo kutoka taasisi mbalimbali za kifedha.

Aidha walisema kumekuwepo na changamoto mbalimbali ambazo zimekuwa zikiwakabili kutoka na wateja wanaofika katika sanamu hiyo na kupiga picha na baadhi yao tutokuzichukua picha izo, ivyo kusababisha hasara kwa kwao na kuwarudisha nyuma kiuchumi.

“Kuna baadhi ya wateja huondoka moja kwa moja baada ya kuwapiga picha kwa ajili ya kumbukumbu zao na hivyo kutufanya tuingie hasara kutokana na gharama za kusafisha picha hizo za wateja’’walisema wapigapicha hao.

Kwa upande wake mmoja wa wageni Gerady Izack kutoka Tanga aliliambia gazeti hili kuwa kumekuwepo na gharama za kupiga picha licha ya eneo hilo kutumiwa bila ya kulipa ushuru wowote ndani ya halmashauri ya jiji na wapiga picha hao.

“Nimeambiwa kila picha moja ni 1000 ukitaka kupiga katika eneo hili la kumbukumbu ya sanamu ya samaki na hiyo ni fedha kubwa kwa Mtanzania wa kawaida tunawaomba wapunguze”alisema Izack.

Pia mmoja wa wafanyakazi wa Kampuni ya Vick- Fish Elizabeth Aron ambaye anahusika na usafi katika eneo hilo alisema kuwa baadhi ya watu wanaofika katika eneo hilo wamekuwa wakikanyaga maua ovyo kutokana na kutofuata utaratibu uliowekwa na kuwa imekuwa ikileta usumbufu wa kulitunza eneo hilo.

Alisema ujenzi wa sanamu hiyo umemwezesha yeye na wenzake kujipatia ajira kutokana na kulipwa kati ya 18,000-30,000 kwa wiki kutoka kampuni hiyo ya Vick Fish ambayo ndiyo yenye jukumu la kutunza eneo hilo.

Kwa upande wake Afisa Biashara wa jiji la Mwanza Sizya Ramadhani alisema kulingana na sheria ya mwaka 1972 wanaruhusiwa kumtoza mtu mwenye eneo maalumu la Biashara na kuwa kwa siku zijazo wataangalia uwezekano wa kuweka utaratibu wa kuwatoza watu wanaofanya biashara katika eneo hilo.

Hatua ya ujenzi wa sanamu ya samaki katika barabara ya Kenyatta jijini Mwanza imepelekea kuwepo kwa kivutio kikubwa kwa wageni mbalimbali toka ndani na nje ya nchi wanaotembelea jiji hilo.

# Mwaloni: Chachu ya ajira kwa vijana jijini Mwanza

**Na David Azaria**




*Soko la kimataifa la Mwaloni lililoko Jijini Mwanza,limeendelea kuwa chanzo cha ajira kwa vijana 600 (Picha na David Azaria).*

Sokola Kimataifa la Mwaloni lililokoJijini Mwanza limekuwa ni chachu ya maendeleo kwa kutoa ajira mbalimbali kwa vijana na makundi mabalimbali ya kijamaa.

Miongoni mwa biashara zinazofanyika ni pamoja na biashara ya kuuza nafaka lakini biashara kuu inayofahamika na ambayo inafanywa na watu wengi ndani ya soko hilo ni Biashara ya kuuza Samaki pamoja na Dagaa.

Baada ya kupata mafunzo ya wiki mbili juu ya habari za uchunguzi wa Biashara na uchumi yanayoendeshwa na Chuo kikuu cha Mtakatifu Augustine Jijini Mwanza na kuwashirikisha waandishi wa habari zaidi ya 30 kutoka katika vyombo mbalimbali vya habari hapa nchini,niliamua kutembelea soko hilo ili kujua ni namna gani limewainua wakazi wa jiji hili kiuchumi hususani vijana.

Nafika katika soko hilo majira ya saa 3:30 asubuhi na moja kwa moja natafuta ofisi ya Mwenyekiti wa soko hilo ili kufanya mahojiano naye,naambiwa hayupo hajafika ofisi,lakini natafuta namba yake ya Kiganjani kutoka kwa mmoja wa wafanyabiashara katika soko hilo,ambaye ananipatia nampigia na baada ya muda mfupi anawasili.

Naketi naye ofisini na baada ya kujitambulisha na kumueleza sababu zilizonifikisha ofisini kwake anajitambulisha kwa jina la Christopher Wankyo naanza mahojiano naye kama ifuatavyo:

**SWALI:**Wewe ni Mwenyekiti wa wafanyabishara katika soko la kimataifa la mwaloni,Tueleze uwepo wa soko hili umesaidia vipi kuinua kipato ama uchumi wa wakazi wa jiji la Mwanza hususani Vijana?

**MAJIBU:**Kwanza soko hili lilianza rasmi kufanya kazi mwaka 2005 baada ya ujenzi wake kukamilika,kwanza tunaipongeza serikali kwa kulijenga soko hili,kwa sababu kabla ya soko hili kujengwa sisi kama wafanyabishara tulikuwa tunapata taabu sana namna ya kuhifadhi mali zetu kwa sababu zilikuwa zinaharibiwa na mvua.

Lakini pia hata wakati wa kuuza bidhaa zetu tulikuwa tunauzia juani na hivyo kujikuta tukiathiriwa na jua,hali iliyokuwa inasababisha matatizo mengine ikiwa ni pamoja na kuugua maradhi ya aina mbalimbali.

Pia vijana wetu walikuwa wanapoteza maisha yao kutokana na kutokuwa na bandari ya kupakia na kupakua mzigo ambapo walikuwa wakilazimika kuogelea ndani ya maji kwa ajili ya zoezi hilo hali ambayo ilikuwa inawasababishia kupata magonjwa mbalimbali ikiwemo Kichocho pamoja na Amiba,na wengi wao kupoteza maisha.

Kuhusu namna gani soko hili limesaidia kuinua uchumi ama kipato cha wakazi wa jiji hili na hasa vijana,ni ukweli usiopingika kwamba uwepo kwa soko hili umeinua uchumi wa vijana wengi kwa sababu umesababisha kuwepo kwa ajira nyingi ambazo zinawafanya vijana kujiingizia kipato na hivyo kuwa na uwezo wa kuendesha maisha yao.

Kama unavyoona shughuli nyingi zinazofanyika hapa ni za usombaji wa Mizigo kutoka Bandarini lakini pia upakiaji,na si hivyo tu hata magunia haya ya Dagaa yanayosafirishwa kwenda nje ya nchi ama mikoa ya kusini ni kazi ngumu zinazohitaji nguvu,na wenye nguvu ni vijana kwa hiyo vijana hapa wananufaika sana na shughuli hizi.

**SWALI:**Kwa kuwa wewe ni Mwenyekiti wa wafanyabiashara katika eneo hili tena kwa muda mrefu hebu tupe takwimu,ni vijana kiasi gani ambao wamejiajiri ama kuajiriwa ndani ya soko hili.

**JIBU:**Kama nilivyosema kwamba shughuli nyingi zinazofanyika hapa zinahitaji nguvu na kuna zaidi ya watu 1000 wanaofanya kazi zao ndani ya soko hili kila siku,ukiangalia zaidi ya asilimia 80 ya watu wanaofanya kazi ni vijana na tunaamini zaidi ya vijana 600 wanafanya kazi humu ndani ya soko na hivyo kujipatia kipato.

Lakini si hivyo tu pia kuna wakina mama ambao ni wajane waliofiwa na waume zao pamoja na wale waliokimbiwa na waume na kuachiwa familia,nao wanafanya kazi humu nadni ya hivyo kujipatia kipato ambacho kinawasaidia kuendesha maisha yao ya kila siku.

**SWALI:**Umesema uwepo wa soko hili umesaidia kuwapa vijana kipato pamoja na kuinua uchumi wao hali ambayo imewawezesha kuweza kumudu kuendesha maisha yao,nini wito wako kwa serikali kwa sababu inavyoonekana idadi ya watu ni kubwa katika soko hili na sasa linaonekana kuwa dogo?

**JIBU:**Ni kweli soko kwa sasa ni dogo wakati linajengwa lililikuwa linaonekana ni kubwa na hata wakati tunaanza biashara hatukuwa watu wengi kiasi hiki,lakini baada ya watu kugundua kwamba hapa ni moja ya maeneo ambayo mtu anaweza kwenda na kujipatia kipato idadi ya watu imekuwa ikiongezeka kila siku.

Na kutokana na hali hiyo sisi kama viongozi wa soko hili tayari tumeiandikia barua serikili kupitia halmashauri ya jiji ili kama kuna uwezekano walipanue kwa sababu kuna eneo kubwa tu ambalo limebaki na kama serikali ikiamua inaweza kuwekeza na hivyo kupanua soko na kuongezeka idadi ya watu.

Baada ya mahojiano na Mwenyekiti huyo niliamua kufanya mahojiano na baadhi ya vijana wanaojishughulisha na shughuli pamoja na biashara mbalimbali ndani ya soko hilo,ambapo baadhi yao wameeleza faida wanazozipata kutokana na uwepo wa soko hilo.

Wakizungumza na Gazeti hili baadhi ya vijana wanaojishughulisha na biashara pamoja na shughuli mbalimbali ndani ya soko hilo ikiwemo upakuaji na upakiaji wa mizigo Bandarini,walisema uwepo wa soko hilo umewafanya kujipatia ajira za kudumu ambazo zinawafanya kumudu gharama za maisha ya kila siku.

"Kwa mfano mimi hapa kazi yangu kila siku ni kukatakata vichwa vya samaki vinavyotoka kiwandani kwa ajili ya kuandaliwa kabla ya kukaushwa na kuepelekwa kwa walaji,naingia asubuhi saa 12 natoka saa 12 jioni au saa moja usiku wakati mwingine hadi saa mbili,lakini ninapotoka hapa nakuwa na fedha yangu taslimu ambayo ni mali yangu kwa kazi nilizofanya siku nzima…." Anasema Mmoja wa vijana hao Enos Lucas.

Anaongeza"hapa kama mzigo unakuwa mkubwa sana basi kwa siku naondoka na shilingi 40,000/=,au 50,000/=,pamoja na kwamba kazi ni ngumu lakini fedha inayopatikana ni nzuri na inasaidia kuendesha maisha ya kila siku kwa sababu tuna familia ambazo zinatutegemea……".

Kwa upande wao John Elias,Zakayo Kingi,na Mabula George wanasema uwepo wa soko hilo umewafanya kupata ajira kwani fedha wanazozipata zimekuwa zikiwasaidia kuendesha maisha yao ikiwa ni pamoja na kusomesha watoto wao pamoja na wadogo zao.

"Kama hili soko lisingekuwepo sijui sasa hivi ingekuwaje,vijana tuko wengi sana humu ndani na tunapata fedha za kutosha kabisa,kama mtu unajituma huwezi kukosa shilingi 20,000/= kwa siku au 40,000/=,na kwa sababu ukitoka hapa unakuwa umechoka unakwenda nyumbani kupumzika hakuna yale mambo ya kujirisha mitaani,na kama hili soko lisingekuwepo basi hali ingekuwa ni tete huko mitaani,ingekuwa ni wizi mtindo mmoja….." anasema Mabula.

# "Likizo (SAUT) imeniathiri kiuchumi" - Beatrice

**Na Antony Mayunga**

"**TOKA** mwaka 2008 nauza magazeti eneo hili ,lakini kila ifikapo mwezi julai hadi Oktoba hali ya biashara huwa ngumu…inafikia wakati natamani kuhama kipindi hicho kinapofika…..''haya ni maneno ya Beatrice Ernest (25).

Beatrice ni Mkazi wa Iseni katika jiji la Mwanza ambaye biashara yake kuu ni ya kuuza magazeti,biashara ambayo anaifanya katika eneo la Chuo kikuu cha Mtakatifu Augustine kilichopo Nyegezi Jijini Mwanza.

Awali Beatrice alikuwa akiuzia magazeti yake eneo la katikati ya jiji la mwanza kabla ya kuamua kuhamishia biashara yake katika eneo la Malimbe kilipo chuo kikuu cha SAUT,chuo chenye jumla ya wanafunzi 12,500,ambapo pamoja na biashara ya magazeti pia amekuwa akitoa huduma za Mpesa,na kuuza vocha za aina mbalimbali.

Katika mahojiano maalum na mwandishi wa makala hii, Beatrice ambae mara zote katika mazungumzo yake na mimi anaonekana mtu aliyekata tamaa anasema hali ya biashara katika eneo hilo inategemea zaidi wanachuo hivyo wakati wa likizo na wengine kuhitimu masomo yao kila mwaka imekua ikimuathiri kiuchumi.

Anasema katika kipindi hicho mauzo hushuka kiasi cha kukatisha tamaa kutokana wanunuzi wanaotoka nje ya chuo kuwa wachache.

"Kibaya zaidi ni kwamba pamoja na mauzo kushuka lakini hali ya maisha inazidi kupanda ambapo inanilazimu wakati mwingine kutumia hadi mtaji niliokuwa nao na ndio maana napata wazo la kuhama kwa muda kwenda eneo lingine"anasema Beatrice.

Anasema alianza na biashara ya kuuza magazeti na kisha baadae kufuatiwa na uuzaji wa vocha ikiwa ni sambamba na utoaji huduma ya kifedha ( M-pesa) ambazo kwa ujumla wateja wake wakufunzi pamoja na wanafunzi katika chuo hicho.

Beatrice anabainisha jinsi mauzo yake kwa siku yalivyokuwa kabla ya hali hilo ambapo anaiita biashara mdororo, huku upande wa magazeti alikuwa akipata sh,30,000 = kwa siku kama faida,vocha tsh,10,000 hadi 15,000= kwa siku na huduma ya Mpesa kwa mwezi alikuwa akipata tsh,350,000 mpaka 400,000 na hii inatokana na kulingana na uwekaji na uchukuaji wa fedha.

"Biashara ya kuuza magazeti ndiyo imezaa na kufuatwa na zingine… hivyo kila siku nimekuwa nikiwaza kuongeza vitu kulingana na mahitaji ya wateja …lakini kwa hali ilivyo kwa sasa naamini wengi wa wafanya biashara wa eneo hili tumeyumba ,wapo walioamua kufunga mpaka mwezi wa kumi"anadai.

Anasema kwa sasa analazimika kuchukua magazeti machache kwa kuwa wateja wake wamepungua ambayo hata hayo machache yamekuwa hayaishi hivyo kufanya faida yake kuwa kidogo na kumlazimu kupunguza kiwango cha mzigo .

"Kabla ya kuondoka wanachuo nilikuwa naleta nakala zaidi ya 30 za magazeti ya Kiswahili … udaku nachukua nakala 10 ambayo pia uhakika wa kuisha ni mdogo…,hapo hapo nalazimika kumlipa msadizi wangu kila siku Tsh,2,000= chakula na mahitaji mengine kwa muda wa miezi mitatu hivyo ni lazima kuyumba "anaeleza.Hata hivyo anasema kuwa mapato hayo yameshuka zaidi ya nusu lakini majukumu yanabaki pale pale,hali ambayo inasababisha maisha kuwa magumu kila siku.




*Beatrice akiwa kwenye eneo lake lakuuzia magazeti chuoni SAUT (Picha na Antony Muyunga)*

"Kwa mfano nasomesha wadogo zangu wawili sekondari, nina mtoto na ndugu wengine… nahitaji kujenga nami niweze kufungua hata miradi mingine naomba uone changamoto ya kiuchumi inavyowakabili wafanya biashara wa eneo hili la Malimbe mimi ni mmoja wao"anafafanua .

Pamoja na kukabiliana na changamoto hiyo ya kiuchumi Beatrice hakuweka kando mafanikio yake kuwa kutokana na biashara hiyo kwa miaka minne tayari amenunua kiwanja eneo la Maina Jijini Mwanza kwa zaidi ya tsh,600,000/=,huku akibainisha kuwa kama biashara ingeenda vizuri angeanza ujenzi.

Anasema matarajio yake baada ya biashara kuimarika anategemea kuongeza huduma za kifedha za Tigo Pesa,Airtel Money ili aweze kushika soko hilo vizuri.

"Kwa sasa naelekeza nguvu zangu kwenye kazi ya ushonaji nguo ninayoifanya kila siku usiku mimi ni fundi cherahani kazi ambayo naifanya usiku sasa nitaelekeza nguvu huko ili kukabiliana na hii hali inayonikabili"anaeleza.

Beatrice anaishauri serikali kushirikiana na wawekezaji wa ndani kuhakikisha wanainua maisha ya watanzani ambapo anasema serikali inatakiwa kuwekeza zaidi kwenye maendeleo ya wananchi na si kujipangia mabilioni ya fedha kwenye posho na chai wakati wananchi wakiendelea kulalamika na kuumia.

# Mafundi seremala wakabiliwa na ushindani kibiashara

**Na Jackson Mollel**

Mafundi seremala jijini Mwanza wanakabiliwa na ushindani mbukwa unaosababishwa na uingizwaji wa samani kutoka nje ya nchi. Hayo yamebainishwa na baadhi ya mafundi seremala walipokuwa wakizungumza na gazeti hili hivi karibuni katika maeneo mbalimbali ya jiji.

Akizungumza kwa niaba ya wenzake Alfred John ambaye ni fundi seremala katika eneo la Furahisha alisema kufuatia uingizwaji wa samani kutoka nje ya nchi biashara yao imekuwa ikidorora kutokana na samani hizo huuzwa kwa bei ya chini.

"Pamoja kwamba samani hizo uonekana kuwa nzuri kwa muonekano na zenye bei nafuu kwa wateja, lakini baadhi ya wateja hao wameshabaini ubora hafifu wa samani hizo ambapo kwa sasa wameanza kurejea kununua samani zinazotengenezwa hapa nchini" alisema Alfred.

Alfred alisema changamoto zingine zinazo wakabili ni pamoja na ukosefu wa mitaji na ukiritimba katika kutoa mikopo pamoja na mali ghafi mbao ambazo huuzwa kwa bei ya juu, jambo ambalo huwafanya wao kuuza samani hizo kwa bei ya juu ikilinganisha na samani kutoka nje ya nchi.

Kwa upande wao, baadhi ya wanunuzi wa samani hizo walibainisha kuwa samani zinazotengenezwa hapa nchini ni imara kuliko za nje na kuwa hulazimika kutozinunua kutokana na bei yake kuwa juu ikilinganishwa na samani za nje.

Mmoja wa wanunuzi hao Lissa Fredi alisema kuwa wao hupenda kununua samani za nje kutokana na upatikanaji wake wa haraka ikilinganishwa na samani za ndani ambazo hazipatikani kwa haraka.

"Upatikanaji wa samani kutoka nje ya nchi kama China na Japani, zikiwemo meza, kabati na viti ni rahisi sana kuzikuta madukani tofauti na samani za ndani ambazo si rahisi kupatikana katika maduka mengi hadi kwa taarifa maalum kutoka kwa mafundi wa samani hizo"alisema Lissa.

Akizungumzia suala hilo mkazi wa eneo la Nyamanoro jijini Mwanza Jonas Imanuel alisema samani za nje huharibika mapema tofauti na zile zinazotengenezwa hapa nchini ambazo mwananchi wa kawaida hawamudu kuzinunua, na kuiomba serikali kupunguza gharama ya malighafi mbao sambamba na ushuru ili mwananchi aweze kununua samani za hapa nchini ambazo ndio imara zaidi.

Kutokana na hali hiyo wajasiria mali hao wameiomba serikali kuzuia uingizwaji wa samani kutoka nje ya nchi kiholela ili kujenga ushindani kwa bidhaa za ndani pamoja na kuwawezesha watanzania kuwa na utamaduni wa kununua bidhaa za hapa nchini kwa lengo la kuinua uchumi wa taifa.

# Bi Aisha mfano wa kuigwa kwa wanawake

**Na Monica John**

Zama hizi ni tofauti sana na zama za kale katika mambo mengi sana mojawapo likionekana kwa upande wa wanawake.

Wanawake walikuwa na majukumu ya kutunza familia na shughuli zote za ndani. Walikuwa tegemezi kwa waume zao. Kama kichwa cha familia, wanaume ndio walikuwa na jukumu la kuhakikisha familia inapata mahitaji yote muhimu kama chakula, mavazi, watoto kwenda shule, matibabu n.k.

Wanawake wa zama hizi wameweza kuonesha mapinduzi. Si tegemezi tena bali amekuwa mstari wa mbele katika kuchangia pato la familia na wakati mwingine kubeba jukumu zima la kuilea familia peke yake inapobidi.

Ujasiriamali umekuwa ni fursa kubwa sana katika kuwainua wanawake kiuchumi kwani wanawake wengi wameweza kujishughulisha na biashara ndogo ndogo tofauti na zamani.

Aisha Issa (36) ni mmoja wa wanawake hao hapa nchini waliochukua hatua madhubuti za kudhubutu kuondokana na dhana ya utegemezi kwa kuwa mjasiriamali wa biashara ya nguo ambazo huziuza mnadani.

Yeye ni mkazi wa wilaya ya Nyamagana jijini Mwanza. Pia ni mfanyabiashara mdogo katika mnada wa Mkuyuni uliopo katika kata ya Butimba wilayani Nyamagana jijini Mwanza, mnada ambao hufanyika mara moja kwa wiki.

Pia ni mama wa watoto wanne wawili wakiwa sekondari na wawili wakiwa shule ya msingi; Amina na Anifa (sekondari) pamoja na Halima na Amisa (shule ya msingi).

Ni miaka mitatu sasa toka alipoanza biashara hii ya kuuza nguo za kike kama sketi, blauzi, shumizi na magauni. Nguo ambazo huzinunua mnadani na baadae kuzishonya (kuzirekebisha)na kuzirudisha tena mnadani kwa kuziuza.

Biashara hiyo imemwezesha kuilea familia yake vizuri baada ya kuachana na mumewe ambae aliondoka kuelekea ukerewa kwa lengo la kutafuta maisha, matokeo yake akahamia huko na kuoa mke mwingine na kuitelekeza familia hiyo.

“Hapa nilipo nasomesha watoto wanne, nimejenga na familia yangu inaishi maisha mazuri kwa kutegemea biashara hii unayoiona ya kununua nguo, kuzishona na kuuza” alisema Aisha.

Biashara hiyo pia imemwezesha Bi Aisha kuchukua mikopo katika taasisi mbalimbali Kwa lengo la kufanyia mambo mengine ya maendeleo mbali kuwekeza mikopo hiyo katika biashara yake.

Kwa mafanikio zaidi, ameweza kukopa mpaka shilingi laki 7 na kuzirejesha bila taabu yoyote.

“Si tu watoto wangu wote wanne wanasoma kwa kutumia mikopo kutoka katika taasisi mbalimbali za kijamii na lakini pia nimeweza kujenga nyumba ninayoishi kwa sasa” alisisitiza

Kutokana na bishara hiyo ya nguo, Bi Aisha alieleza kuwa kwa siku kama biashara ikienda vizuri anaweza kuuza mpaka shilingi laki moja na kuwa akiuza chini sana ni shilingi elfu 30.

Haikuwa rahisi kwa mwana mama huyu kuianzisha biashara hiyo na kufika ilipo fika hivi leo.

“Nilianza biashara hii kwa mtaji wa shililingi elfu 10. Na kwa mara tatu mfululizo mtaji huu ulikufa kutokana na wateja kunirusha. Si kukata tamaa nilidhubutu tena na sasa biashara yangu imesimama na ndo kitega uchumi pekee cha familia yangu”

Licha ya biashara yake hiyo kuonekana duni machoni mwa watu hasa kwa wanawake wengine kwa maelezo ya mjasiriamali huyo, yeye hakuweza kuikatia tamaa hasa baada ya kuona hali ya familia inazidi kuwa ngumu na kuwa yeye ndio tegemeo.

Bi Aisha yeye ana ujuzi wa kushona(fundi cherehani) na kwa kuwa kabla ya kujiunga katika biashara hiyo alikuwa anashona nguo na kuwauzia watu wakati mwingine kwa kuwakopesha.

Kazi hiyo haikuwa na faida tena na hivyo hakuweza kuendelea nayo kutokana na kuwadai watu wengi jambo ambalo liliuwa mtaji wake huo.

Hapo ndipo ambapo, Bi Aisha aliamua kuchukua hatua na kuanza kufanya biashara ya kununua na kuuza nguo katika minada, biashara ambayo imeweza kumpatia wateja wengi na hivyo kuwa na faida.

Palipo na mafanikio, changamoto hazikosekani. Bi Aisha alieleza changamoto mbalimbali ambazo amekumbana nazo katika biashara hiyo mbali na mafanikio mbalimbali ambayo ameweza kuyaainisha.

Mojawapo likiwa ni suala la kutokuwa na maeneo maalumu ya kufanyia biashara zao jambo ambalo linawapelekea kufukuzwa na mgambo jiji wakati wakiwa wanafanya biashara zao katika maeneo katikati ya jiji.

“Halmashauri ya Nyamagani imekuwa haiwajali wajasiriamali wadogo wadogo, hususani ni katika kuwatengea maeneo ya kufanyia biashara zao inafikia tunalazimika kukimbia tunapowaona migambo kwa hofu ya kukamatwa na kufunguliwa mashtaka ya kufanyia biashara katika maeneo yasiyoruhusiwa”alilalamika

Katika kuonesha ugumu wa kufanyia biashara katika maeneo waliyowekewa kufanyia biashara, Bi Aisha alifafanua kuwa maeneo hayo si tu yapo mbali na mji bali pia barabara ni mbaya na hivyo kupelekea usafiri kuwa mgumu kwa wafanya biashara hao pamoja na wanunuzi wa bidhaa zao kufika huko.

“Kweli taasisi ambazo tunazitegemea kutupatia mikopo zimekuwa zikiweka masharti makubwa pamoja na kutoza riba kubwa,hivyo wafanyabishara kujikuta wanaogopa kukopa au wanashindwa kurejesha mikopo hiyo”Aliongezea changamoto.

Hata hivyo, licha ya kutozwa ushuru wa shilingi 200 wanapokuwa mnadani, bado mazingira wanayofanyia biashara si mazuri na wakati mwingine hata vyoo vinakuwa ni tatizo.

Sehemu za kuweka biashara zao pia imekuwa ni tatizo mpaka inafikia ugomvi kati ya wafanya biashara kutokana na kuwa hakuna sehemu maalumu kwa mfanya biashara fulani mpaka mfanyabiashara huyo aweze kuitumia sehemu husika kwa muda mrefu ndipo atakapoihalalisha kuwa yake.

Kwa upande wa bei, wateja wamemekuwa wakitaka kupunguziwa nguo hizo kwa bei ambayo Bi Aisha anasema kuwa ni ya hasara kutokana na gharama anazopata kuanzia kwa kununua na kuzishona tena zionekane vizuri kwa mauzo.

“Wakati mwingine unakuta nguo umenunua shilingi 2000 nimeipunguza na kuiboresha ninapoileta sokoni kuja kuiuza natakiwa niuze shilingi 3000 lakini mteja anapokuja kununua anataka umpunguzie umuuzie kwa bei ya chini mpaka shilingi 500”Analalamika.

**Matarajio yake**

Bi Aisha alieleza kuwa ana mpango wa kujenga nyumba kwa ajili ya kukodi kwa ajili ya kuongeza kitega uchumi kwa familia yake hiyo.

Hata hivyo, kuonesha kuipenda na kuithamini kazi yake, Bi Aisha alifafanua kuwa hana matarajio ya kuiacha biashara yake kwani ndiyo aliyoizoea.

“Hii biashara nimeizoea na ipo kwenye damu,hivyo siwezi kuacha nikafanya biashara nyingine labda ikatokea mtu akiniongezea mtaji kwenye mtaji niliona nao ningeweza kufanya vizuri zaidi na kukidhi mahitaji ya wateja wangu”Alibainisha.

**Wito.**

Zaidi Bi Aisha anawaasa wanawake waamke na kujishughulisha kuliko kuwa tegemezi kwani kuna leo na kesho yawezekana yakatokea yaliyomkuta yeye.

Anasema kuwa ifike wakati wanawake nao wawe mstari wa mbele katika kujishughulisha na kazi mbalimbali za ujasiriamali ambazo zinaweza kuwasaidia,hata kama wanaume nao watakuwa na kazi zinawaingizia kipato kwani anaamini kuwa wakithubutu wanaweze kufika mbali sana kimaendeleo.

Kwa upande wa uongozi wa Jiji, mjasiriamali huyu anatoa wito kwa uongozi kuhakikisha kuwa wanawekewa mazingira mazuri yatakayowawezesha wafanyabiashara wadogo kunifaika.

# Uhaba wa mninga waleta changamoto nchini

**Na Kareny Masasy**

Ingawa kuna miti ya aina nyingi inayotumika katika utengenezaji wa samani za majumbani na maofisini, mti wa aina ya mninga umekuwa "lulu" ndani ya jiji la Mwanza kutokana na ubora wake.

Mti huo mbali na kutopatikana kirahisi baadhi ya mafundi selemala wanauhitaji mti huo kutokana na samani zinazotengenezwa kutokana na mti huo kuwa ni imara, bora na ng'avu.

Mti wa mninga ambao haupatikani kirahisi katika jiji la Mwanza asili yake ni porini (mti pori) na hupatikana katika baadhi ya maeneo ya mkoa wa Tabora, Kagera na Ruvuma.

Kwa kawaida mti huu hauna sifa ya kupandwa nyumbani kama ifanywavyo miti mingine au kuota sehemu yoyote jirani na kaya.

Mmoja wa mafundi selemala Bernad Ochieng (32) mkazi wa eneo la Mkuyuni jijini Mwanza anasema kuwa kutokana na mbao za mti wa mninga kuwa adimu baadhi yetu tunalazimika kutumia mbao aina ya *cypress* na mtundu ambazo hazina ubora.

"Mbao ya mninga ikipatikana huuzwa bei ya ghali lakini pia hutumiwa zaidi kwa kutengeneza milango na madirisha jambo ambalo hutoa ushindani mkubwa kwa mafundi wa vifaa vya ndani" anasema Ochieng.

Ameongeza kuwa kutokana na mbao za mti huo kuuzwa kwa bei kubwa hata wao hulazimika kuuzwa samani wanazotengeneza kwa bei ya juu.

" Kitanda cha futi tatu na nusu ninakiuza shilingi 80,000 na cha futi tano kwa sita nakiuza kwa shilingi 170,000 iwapo ninatumia mti wa *Mtundu* au *Cypress*,' anasema.

'Kama nitatumia mti wa mninga bei ya samani hizo hupanda kutokana na hali halisi ya ubora wa mti na upatikanaji wake hivyo hulazimu kupandisha bei kwa gharama ya shilingi 180,000 kwa kitanda cha futi tatu na nusu na cha tano kwa sita hutoza shilingi 280,000,' Anasema .

Anasema kuwa analazimika kuuza bei hiyo kutokana na ukweli kuwa vitu vinavyotengenezwa kwa mbao za mninga hudumu hata kwa miaka 100 tofauti na vya *Cypress* na mtundu.

Hata hivyo, Ochieng anasema kuwa pamoja na kutengeneza vifaa vyao kwa kutumia mbao inayopatikana kirahisi bado wanakabiliwa na changamoto ya kupata soko kutokana na ongezeko la bidhaa za kutoka nchini China ambazo huuzwa kwa bei ya juu.

Amesema kuwa tatizo hilo linatokana na mtizamo wa wananchi kuona vifaa vya kutoka nje ya nchi kuwa ni vizuri zaidi kuliko vinavyotengenezwa hapa nchini hata kama havidumu.

"Vitu vinavyotoka nchini China vinatengenezwa kwa chuma na huuzwa kwa bei kubwa lakini ndivyo wananchi wanavyovikimbilia ,'Anasema ochiengi na kuongeza kuwa

"Vitu vya china huaribika kwa haraka lakini utengenezaji wake ni wa shida kwa kuwa vifaa vya kurudishia havipatikani sana madukani,"anasema Ochieng.

Naye, Bi Hadija Luhende mkazi wa jijini Mwanza anasema kuwa analazimika kutumia vifaa vya wachina ingawa vinauzwa kwa bei kubwa kutokana na kukosekana kwa mbao imara za mti wa mninga.

Anasema kuwa vitu vinavyotengenezwa kwa mbao nyingine uharibika mapema kutokana na kuliwa na wadudu jambo ambalo husababisha kupoteza uhalisia wa kitu husika.

Mfanyabiashara wa vifaa mbalimbali kutoka nchini China, Mustapha Ally hivi sasa mauzo ya bidhaa zetu yameongezeka ikilinganishwa na miaka ya nyuma.

"Siku za nyuma tulikuwa tunauza vitanda viwili kwa wiki tatu mpaka mwezi lakini sasa idadi ya wateja imeongezeka na kufikia vitanda kati ya tano hadi kumi kwa muda huo," anasema.

Amesema kutokana na ongezeko la mauzo hata faida wanayopata ni kubwa tofauti na siku za nyuma.

Aidha amefafanua kuwa kitanda kimoja cha kutoka nchini china kinauzwa kwa shilingi millioni 1.3 , viti sita na meza yake vinauzwa kwa shilingi 540,000 huku kabati lenye milango miwili midogo linauzwa kwa kiasi cha shilingi 300,000.

Naye, balozi wa china Lv Youqing anasema kuwa nchi ya China imetoa nafasi 400 kwa wajasiriamali wa Tanzania kupeleka bidhaa zao nchini China bila ya kulipia ushuru wowote.

Hivi karibuni Waziri wa viwanda na biashara Dk. Abdala Kigoda amewataka wafanyabiashara wa Kitanzania kuwa wabunifu kwa kutengeneza bidhaa bora ili kupanua wigo wa soko la kibiashara ndani na nje ya nchi.

Hata hivyo, baadhi ya wadau mbalimbali wa masuala ya uchumi wameiomba serikali kutosafirisha miti ya mininga kwenda nje ya nchi kwa wingi ili itumike humu nchini kutengeneza bidhaa mbalimbali.

Wachumi hao wamesema kuwa hatua hiyo itawasaidia mafunzi selemala kutengeneza bidhaa zenye ubora ambazo zitakubalika katika soko la ndani na nje ya nchi na hivyo kusaidia kutoa ajira zaidi kwa watanzania na kuongeza pato la taifa kwa ujumla.